BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MIUNDOMBINU, ARDHI NA TEHAMA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Nianze kwa kumshukuru **Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema na utukufu,** kwa kutujaalia uhai na Afya njema, na kutuwezesha kukutana tena katika Baraza hili la Kumi na moja Mkutano huu wa Tatu, kwa dhamira ya kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar ambao ndio sababu ya sisi kusimama katika Baraza hili, nasi hatuna budi kurejesha imani kwao kwa kuwatumikia kwa dhati na kwa moyo wetu wote, kwa dhamira ya kutetea maslahi yao katika Baraza hili tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekeee nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi** kwa uongozi wake wa busara ulojaa hekima kwa jitihada anazochukua katika kuendeleza na kuboresha Miundombinu mbali mbali nchini ikiwemo Miundombinu ya maji na Nishati kama

Umeme pamoja na Ujenzi na Uboreshaji wa Miundombinu mbali mbali nchini kwa lengo la kuwaletea maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Pia, nimpongeze **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla** Makamo wa Pili wa Raisi ambaye ndiye msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali katika chombo hichi muhimu cha kutunga sheria cha Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwa kumsaidia vyema Mheshimiwa Rais wetu katika kutekeleza majukumu yake ya kuiongoza nchi hii, pamoja na jitihada anazozichukua katika kuhakikisha analeta maendeleo na mabadiliko ya kasi kwenye kuimarisha upatikanaji wa huduma za maji, Nishati na Madini na kuweka mikakati maalum kwenye maliasili zisizirejesheka kupitia Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Nichukuwe fursa hii kukupongeza wewe **Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid** kwa kuaminiwa tena na wajumbe wa Baraza hili na kukuchagua kuwa kiongozi wetu ndani ya Baraza hili. Lakini pia nikushukuru wewe binafsi Mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii adhimu ya kuwasilisha hotuba hii ya maoni ya Kamati ya kudumu ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Aidha,** Kwa dhati nawapongeza wasaidizi wako Naibu Spika **Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma** pamoja na **Waheshimiwa Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi** kwa umoja wenu kwa jinsi mnavyoendelea kuliongoza Baraza hili tukufu kwa hekima, ustadi na upeo mkubwa. Ni imani yangu kwamba mtaendelea kutuongoza kwa uadilifu na ustadi wa hali ya juu kwa lengo la kuimarisha demokrasia katika chombo hiki muhimu cha kuwatumikia wananchi.

**Mheshimwa Spika,** Kwa niaba ya wajumbe wenzangu wa kamati ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA napenda kutoa pongezi na shukran za dhati kwa Waheshimiwa wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano tuliyokuwa nayo tokea kuchaguliwa kwetu kuwa wajumbe katika Baraza hili Tukufu, Namuomba Allah (S.W) atuzidishie mashirikiano na wepesi katika kutekeleza majukumu yetu tunayopaswa kuyatekeleza kikatiba katika kipindi chetu chote cha uongozi wetu.

**Mheshimiwa Spika,** Shukrani za pekee nazitoa kwa Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA ambao kwa pamoja tumeweza kujadili kwa kina mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hii ya Maji, Nishati na Madini na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha mipango ya fedha zinazoidhinishwa zinalenga matumizi yenye ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Heshima kubwa Naomba uniruhusu niwatambulishe Waheshimiwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Mihayo Juma N'hunga | Mwenyekiti, |
| 2. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | M/Mwenyekiti, |
| 3. Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Mjumbe, |
| 4. Mhe. Prof. Omar Fakih Hamad | Mjumbe, |
| 5. Mhe. Khamis Mohammed Amran | Mjumbe, |
| 6. Mhe. Abdullah Kambotwe Abdullah | Mjumbe, |
| 7. Mhe. Said Ali Mbarouk | Mjumbe, |
| 8. Ndg. Rahma Kombo Mgeni | Katibu, |
| 9. Ndg. Bakar Makame Haji | Katibu, |
| 10. Ndg. Adam Maulid Simai | Afisa Bajeti. |

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka. Hivyo, katika kutekeleza jukumu hilo lililoelezwa na kanuni ya 101 fasili ya kwanza ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2024, Kamati ilikaa kikao na Wizara hii ya Maji, Nishati na Madini ambapo Kamati ilikaa, kuijadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na leo hii

kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati nawasilisha Maoni ya Kamati kuhusiana na mapendekezo ya Bajeti hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Maji, Nishati na Madini iliidhinishiwa **TZS. 220.82 Bilioni,** na kukadiriwa kukusanya **TZS. 20.75 Bilioni** kupitia vyanzo vya mbali mbali. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 Fungu la Wizara liliingiziwa jumla ya **TZS. 87.15 Bilioni** sawa na **asilimia 39.47** ya makaddirio ya Wizara na imeweza kukusanya jumla ya **TZS. 15.29 Bilioni** sawa na **asilimia 75** ya makadirio ya makusanyo kwa mwaka.

Licha ya kazi kubwa inayofanyika katika Wizara hii hasa za Kuhudumia jamii, Kamati imebaini uingizwaji mdogo wa fedha za matumizi na za miradi ya maendeleo kutoka Wizara ya fedha jambo ambalo limepelekea kupungua kwa ufanisi katika utekelezaji wa majukumu muhimu ya Wizara hii ikiwemo kukosekana kwa usimamizi mzuri kwenye masuala ya upatikanaji wa uhakika wa maji, nishati na maliasili zisizo rejesheka kwa ujumla wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Maji, Nishati na Madini ina Fungu Kuu moja ambalo ni **015** ambalo litatekeleza **Programu Kuu tatu (3)** zenye **Programu Ndogo sita** (6). Ili kuiwezesha Wizara kutekeleza Programu

zake hizo na kazi za huduma zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara imeikadiriwa jumla ya matumizi **TZS. 475.39 Bilioni** na makusanyo **TZS. 25.72 Bilioni** kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato. Hivyo kamati inaishauri Wizara ya Fedha kuipatia Wizara fedha ambazo zimekadiriwa tena kwa wakati ili kufikia malengo ya Serikali ya utekelezaji wa miradi iliopangwa na kuweza kutatua changamoto za wananchi kwenye masula ya Maji, Nishati na Madini zikiwemo Mali Asili zisizorejesheka.

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia vikao vya kamati na Wizara katika kujadili mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hii ya Maji, Nishati na Madini Kamati imebaini uwepo wa ongezeko la kibajeti kwa baadhi ya vifungu katika Programu Kuu pamoja na huduma zake na kupelekea ongezeko kubwa la Bajeti katika fungu kuu la Wizara **kutoka TZS. 220.82 Bilioni** kwa mwaka 2025/2026 mpaka **kufikia TZS. 475.39 Bilioni** kwa mwaka 2026/2027 ambayo ni zaidi ya asilimia mia moja ya ongezeko la makadirio ya Wizara kwa mwaka. Kamati iliarifiwa kuwa sababu kubwa ya ongezeko hilo ni uimarishwaji wa miundombinu ya maji na umeme Unguja na Pemba pamoja na miradi itakayotekelezwa kupitia sekta ya maji na Nishati kwa ajili ya maandalizi ya Kombe la Mataifa ya Afrika 2027 (AFCON) ambapo Zanzibar ni miongoni mwa wenyeji wa mashindano hayo.

Kwa kuwa utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2025/2026 kifedha ulikua na asilimia 39.47 tu, Kamati ilikubaliana na mapendekezo ya Wizara juu ya ongezeko hilo.

## PROGRAM KUU YA USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI (P01)

Program kuu hii imeundwa na program ndogo moja ambayo ni Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji **(S0101)** yenye lengo la kusimamia Upatikanaji wa Maji Safi na Salama kwa wananchi inayotekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Maji pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA). Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 programu hii iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS. 165.51 Bilioni** ambapo Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 programu hii ilipatiwa **TZS. 14.67 Bilioni** sawa na **asilimia 8.86** ya makadirio.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Program kuu hii imekadiriwa kutumiwa **TZS. 179.92 Bilioni** sawa na **asilimia 37.85** ya Bajeti ya Wizara. Kamati inaishauri Wizara kuipatia fedha za kutosha Programu hii kwani imebaini changamoto kubwa ambazo zilizorotesha utekelezaji wa kazi za kawaida pamoja na za miradi kutokufanyika kwa ufanisi ilikua ni uingiziwaji mdogo wa fedha kwa ajili ya matumizi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ambayo imekasimu Mamlaka yake kwa Kampuni ya Rand Water Zanzibar ambapo kwa kipindi cha Julai - Machi, 2025/2026 Rand Water Zanzibar ilipanga kukusanya jumla ya **TZS. 13.28 Bilioni** na kufanikiwa kukusanya **TZS. 9.1 Bilioni** zilizotokana na mauzo ya maji na mapato mengineyo sawa na asilimia 68.4 ya makadirio ya mwaka. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha wanaisimamia ipasavyo Kampuni hii ya Rand Water ili kutoa huduma bora kwa jamii ya upatikanaji wa maji mijini na vijijini na kuiongezea mapato Serikali kupitia makushanyo yao.

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya maji ni sekta muhimu na ndio muhimili wa afya kwa umma na ustawi wa jamii, kupitia kifungu cha huduma cha Kusimamia Huduma na Upatikanaji wa Maji Safi na Salama **(H010101)** ambacho kilikadiriwa kutumia ***TZS.* 155.13 Bilioni** Kamati inaitaka Wizara kukitumia vizuri kifungu cha huduma hii kwa lengo la kuendeleza jitihada za Serikali katika kuhakikisha wananchi na wakaazi wa Zanzibar wa mjini na vijijini wananufaika na huduma za maji safi na salama majumbani na sehemu zao za makaazi na biashara ili waweze kutekeleza miradi mingi zaidi waliojipangia katika program hii kama vile mradi wa uchimbaji visima kwa maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba sambamba na utekelezaji wa mradi wa utengenezaji Matanki ya maji ya kisasa ya Zink Aluminium kwa

ajili ya kuhifadhia maji kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma hii ya maji safi kwa wananchi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwekwe mazingira rafiki na uzio kwa sehemu iliyozunguka miradi yote ya maji ili kuzuia maji ya mvua na uchafu kuzunguka matank na visima hivyo pamoja na kuepusha uharibifu unaoweza kufanywa na wale wachache wasiokwa na nia njema ya maendeleo ya nchi. Pia Wizara kupitia kampuni ya Rand Water wawatumie wataalamu wao waweke mifumo ya "automation" kwenye uwekaji wa "chlorine" katika matanki hayo ya maji ili utibuji wa maji uwe wa uhakika na uepuke makosa ya kibinaadamu yanayoweza kutokea.

## PROGRAMU KUU YA USIMAMIZI WA HUDUMA YA NISHATI NA MADINI (P02)

**Mheshimiwa Spika,** Programu kuu hii imeundwa na Program ndogo mbili ambazo ni Program ya Usimamizi na uimarishaji wa huduma za nishati **(S0201)** na Program ndogo ya Usimamizi na uimarishaji wa huduma za madin **(S0202)** ambazo inatekelezwa kupitia Idara ya Nishati na Madini, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) pamoja na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO).

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Program kuu hii iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS. 52 Bilioni** kwa ajili ya matumizi. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 Programu kuu hii imetumia **TZS. 70.39 Bilioni** sawa na **asilimia 135**, ambapo Kwa mwaka wa Fedha 2026/2027 Program kuu hii imekadiriwa kutumia **TZS.291.37 Bilioni** sawa na **asilimia 61.29** ya makadirio ya Wizara ambayo kuna Ongezeko kubwa la makadirio kwa kulinganisha na mwaka wa fedha uliopita wa 2025/2026 ambapo kamati iliarifiwa sababu kubwa ni matayarisho ya kombe la mataifa ya Afrika (Afcon) kwenye matumizi ya nishati ya umeme.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Shirika ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS. 265.32 bilioni** kutokana na mauzo ya umeme na mapato mengineyo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2026 ZECO imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS. 175.65 bilioni,** sawa na asilimia **66.20** ya makadirio ya mwaka na wastani wa **asilimia 103** ya makadirio ya kipindi cha miezi tisa. Aidha, ZECO imetumia jumla ya **TZS. 180.48 bilioni** kwa kazi za maendeleo, mishahara na matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** Nishati ni uhai wa kila kitu tunachokifanya, bila nishati hakuna maendeleo yeyote yatakayokuwepo ya kiuchumi, kijamii, kiusalama na mawasiliano pia. Kwa kujua hilo

kamati kupitia kifungu cha huduma cha Kusimamia Upatikanaji na Kuimarisha Huduma za Nishati nchini **(H020101)** ambacho kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kimekadiriwa kutumia **TZS. 289.83 Bilioni**. Kamati inaishauri Wizara husika kukipatia fedha kifungu hichi kama zilivokadiriwa ili kuwezesha huduma zilizopangwa za upatikanaji wa nishati kwa wananchi zipatikane kwa uwepesi na urahisi na pia kufanikisha utekelezaji wa miradi iliyopangwa ya matayarisho ya Afcon 2027.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi bora ya nishati katika ngazi za mikoa, wilaya na shehia, kwa lengo la kuongeza uelewa juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia na nishati jadidifu. Kamati kadhalika inaishauri jamii kuwa na uwelewa wa kutosha kabla ya kutumia nishati hizo ili kuepusha athari zinazojitokeza mara kwa mara kwa kukosa uweleza wa matumizi kwa Nishati hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia vikao na mahojiano baina ya kamati na Wizara hii, Kamati ilitaka kujua sababu hasa za umeme kuzimika mara kwa mara visiwani hapa ambapo iliarifiwa kuwa mifumo ya zamani ambayo ilikua ikitumika kusambazia umeme kama vikombe na transfoma pia kuja kwa umeme mkubwa pamoja na hitilafu za miti zilizopo kwenye laini kuu ya kusafirishia umeme ni miongoni mwa sababu kubwa za

changamoto ya kuzimika umeme mara kwa mara visiwani hapa ambapo kwa sasa tayari kumechukukuliwa jitihada za kuondosha tatizo hilo kwa asilimia kubwa kwa kuweka vifaa vya kisasa na kubuni njia mbadala. Kamati imeitaka Wizara kuchukua jitihada zaidi kwa kuwatumia wataalamu wao kuhakikisha wanaondoa kabisa changamoto za upatikanaji wa Umeme ili huduma hii iweze kupatikana bila malalamiko kwa wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza wizara kupitia shirika la umeme ZECO kwa jitihada wanozichukuwa za kutatua changamoto za uhaba wa umeme hapa Zanzibar ikiwemo utekelezaji wa miradi mbali mbali kama vile Mradi wa kutatua changamoto za umeme na kuimarisha gridi ya taifa (STATCOM) kwa Unguja na Pemba, Mradi wa kuzalisha umeme wa jua na Betri za kuhifadhia umeme, Mradi wa kuzalisha umeme wa upepo, Mradi wa kuimarisha sekta ya nishati na upatikanaji wa huduma ya umeme (ZESTA) na mradi wa kusafirisha umeme kupitia waya wa Baharini kutoka Tanzania Bara hadi Zanzibar unaosimamiwa na TANESCO wakishirikiana na ZECO.

Aidha, licha ya jitihada hizo kamati inaishauri Wizara kupitia Zeco kufanya tafiti zaidi hasa kwa nchi ambazo zilizoendelea kama Ujerumani na China ili kuhakikisha kuwa tunazalisha Upatikanaji wa Huduma ya umeme unakuwa wa kutosha na

endelevu Ili kufikia malengo ya miradi yaliokusudia na Serikali kwa maslahi ya wananchi wa Zazibar.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwepo kwa madeni makubwa na ya muda mrefu ambayo Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) wanazidai taasisi mbali mbali zikiwemo taasisi za Serikali, hivyo kamati imeona ni vyema kwa Wizara kulisimamia suala hili kwa kuweka utaratibu mzuri utakaowezesha kulipwa madeni haya kama kuanzishwa kitengo maalumu kitakachosimamia madeni kwa kuratibu na ufuatiliaji wa madeni ya wizara ili kuliwezesha shirika na taasisi nyengine za Wizara ziweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi na kupelekea ongezeko la gawio Serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, Suala la mafuta limekuwa ni changamoto kubwa duniani kutokana na hali za kiusalama wa nchi mbali mbali, Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa jitihada zake mbali mbali za kuwarahisishia wananchi juu ya kupata huduma hizi za mafuta tena kwa bei nafuu ukilinganisha na uhalisia wa soko la bei za mafuta lilivyo kwa sasa. Pia kamati inashauri Serikali kupitia Wizara kuhakikisha inaweka miundombinu mizuri na rafiki hasa katika maeneo ya visiwa vidogo vidogo kwa ajili ya kuhifadhia mafuta mengi zaidi ili kupambana na changaoto hii inayoisumbua dunia kwenye nishati hii muhimu kwa maendeleo ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kupitia kifungu cha huduma cha kusimamia Huduma na Upatikanaji wa Madini (H020201) ambacho kimekadiriwa kutumia jumla ya **TZS. 1.55 Bilioi** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Kamati inashauri Wizara kuzitumia vizuri fedha za kifungu hiki cha huduma ili kuhakikisha huduma za Maliasili Zisizorejesheka kwa wananchi wenye uhitaji zinapatikana kwa urahisi na kwa wakati pamoja na miradi ya kimkakati iweze kufanyika kwa ufanisi.

Aidha, Kamati inashauri kutumia Bajeti ya kifungu cha huduma hii kwa kuchukua jitihada za makusudi juu ya kuihuisha ardhi kwa kupanda miti kwa zile sehemu zilizoathitika na uchimbaji wa Maliasili hizo ili kuhakikisha ardhi inakua katika uhalisia wake na kupunguza athari za kimazingira zinazoweza kujitokeza hasa wakati wa mvua kubwa. Vile vile Kamati imeitaka Wizara kuhakikiahsha wanaendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya athari zitokanazo na uchimbaji holela wa maliasili zisizorejesheka.

## PROGRAMU KUU YA URATIBU WA MIPANGO, UENDESHAJI NA UTAWALA WA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI (P03)

**Mheshimiwa Spika,** Programu hii imeundwa na program ndogo tatu ambazo ni Program ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara **(S0301),** Program ndogo ya Utawala na

Uendeshaji wa Wizara **(S0302)** na Program ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara – Pemba **(S0303)** ambazo zinatekelezwa chini ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti pamoja na Afisi Kuu - Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, programu hii iliidhinishwa kutumia jumla ya **TZS. 3.30 bilioni.** Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2026, programu hii imetumia jumla ya **TZS 2.28 bilioni** ambapo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 program kuu hii imepangiwa kutumia jumla ya **TZS. 4.1 Bilioni** sawa na **asilimia 0.86** ya makadirio ya Bajeti ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imearifiwa juu ya Ongezeko la makadirio ya bajeti kwenye Program kuu hii kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kuwa Ongezeko hilo limetokana na kuimarishwa kwa fedha za OC pamoja na malipo ya deni la ulinzi wa visima vya ZAWA kwa Wakala wa Ulinzi wa JKU, hivyo kamati inaishauri Wizara kuimarisha ulinzi sehemu zote zenye miradi ya maendeleo ili kuilinda miradi hiyo kutokana na uharibifu unaoweza kujitokeza.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inaendelea kusisitiza kwa taasisi zinazojitegemea ambapo kutokana na utaratibu uliopo sasa na kwa mujibu wa Takwa la Sheria namba 6 ya mwaka 2021 ya Msajili wa Hazina kifungu cha 26 (1) b, Bajeti zake zinapitishwa

na bodi zao na kamati haipati fursa ya kuzipitia lakini pia hata katika randama la Wizara hazionekani, Kamati inashauri Serikali kuliangalia kwa kina suala hili kwani linaleta ukakasi hivyo kuwekwe utaratibu maalum kwa Kamati kuzipitia bajeti za Taasisi hizo mara tu zinapoandaliwa ili kupata fursa ya kushiriki na kutoa ushauri kwa bajeti hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara kuhakikisha wanafanya utafiti wa kina juu ya miradi wanayotaka kuitekeleza na pia kuwashirikisha wataalamu husika tokea mwanzoni mwa miradi ili kuepusha kufeli kwa miradi hiyo au kuengezeka kwa gharama zisizo za lazima zinazotokana na kukosa ushauri wa kitaalamu tokea mwanzoni mwa miradi husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inawashauri wanajamii na wananchi kwa ujumla hasa kwa wale wanaozungukwa au waliopo karibu na miradi ya maendeleo kama miundombinu ya umeme, miundombinu ya maji au miundombinu mingine yeyote ile juu ya kuthamini jitihada za Serikali kwa kuitunza na kuilinda miundombinu hiyo iliyowekwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa jamii ili kuiwezesha miradi hiyo kuhudumia jamii kwa muda mrefu na kuzidi kupiga hatua za kimaendeleo ndani ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho kabisa napenda kuwashukuru viongozi wote wa wizara hii wakiongozwa na Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar, **Mheshimiwa Nadir Abdul-latif Al-wardy,** pamoja na Naibu Waziri **Mheshimiwa Seif Kombo Pandu,** Katibu Mkuu, Naibu katibu Mkuu pamoja na Watendaji wake wote wa Wizara hii kwa mashirikiano waliyotupatia Kamati yetu wakati wa kupitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara yao, Tunawaomba wazidishe mashirikiano baina yao ili kwa pamoja wazidi kufanikisha malengo ya Serikali kupitia Wizara yao hii kwenye kutoa Huduma bora zikiwemo hudua za Umeme na Maji nchini.

Vile vile, napenda kuchukua fursa hii tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Kamati imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waiunge mkono Bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kusema hayo machache, Kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA naunga mkono hoja.

**Mheshimiwa Spika,** Naombe kuwasilisha.

Ahsante,

…………………………………………

Mihayo Juma N'hunga,

Mwenyekiti,

Kamati ya Miundombinu, Ardhi na TEHAMA,

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR.**